# UENDELEZAJI WA VIKUNDI VYA WAKULIMA





TARP II SUA PROJECT

# UENDELEZAJI WA

# VIKUNDI VYA WAKULIMA

## KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI

Warsha ya Nane ya Wakulima wa Kanda ya
Nyanda za Juu Kusini
Iliyofanyika Ukumbi wa Allamano wa Vijana wa
Kikatoliki Makambako, Njombe
7-9 Juni 2004

---

21 JUL 2017

**Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania**

*(TARP II-SUA Project)*

Juni 2004

**Imeandikwa na**

Bi. Fausta Vallery
Bw. Elimpaa Kiranga
Prof. R. E. Malimbwi
Dk. Joyce G. Lyimo-Macha

**Na Kuhaririwa na**

Prof. L. D. B. Kinabo Mratibu

**ISBN: 9987 – 422 – 04 - 7**

**Kimechapishwa na**

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania (TARP II-SUA Project)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
SLP 3151
Morogoro
Simu: +255 23 2600970 au +255 23 2603511 ext. 1102

Toleo namba: TS2-114

# YALIYOMO


**Dibaji** v

**Vifupisho** vi

**1.0 UTANGULIZI** **1**
- 1.1. Madhumuni ya warsha 1
- 1.2. Ufafanuzi wa maneno 1
- 1.3. Matarajio na hofu ya warsha 2
- 1.4. Mbinu zilizotumika 3

**2.0 UMUHIMU WA VIKUNDI NA UUNDAJI WAKE** **6**
- 2.1. Kuunda vikundi 7
- 2.2 Mambo ya kuangalia katika uundaji 7
- 2.3. Ukuaji wa kikundi 8
- 2.4. Uundaji wa mtandao 9

**3.0 MISINGI YA VIKUNDI BORA** **11**

**4.0 TABIA MBALIMBALI ZA WATU KATIKA VIKUNDI** **12**
- 4.1. Maana ya tabia 12
- 4.2. Aina za tabia za watu katika jamii 12
- 4.3. Migogoro/migongano 13
- 4.4. Chimbuko la migogoro katika vikundi 15

**5.0 KATIBA YA KIKUNDI** **18**

**6.0 MAPENDEKEZO YA KUBORESHA VIKUNDI** **20**

7.0 HITIMISHO 20
7.1. Mipango ya utekelezaji 20
7.2. Tathmini ya warsha 20
7.3. Kufunga warsha 20

8.0 VIAMBATISHO 23
8.1. Orodha ya washiriki 23
8.2. Hali na malengo ya vikundi 25
8.3. Mipango ya utekelezaji wa kazi 29

# DIBAJI

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula (MAFS), na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway (NLH), kinatekeleza mradi wa Utafiti wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania. Mradi huu ambao ulianza rasmi mwezi Septemba 2000, unagharamiwa na Serikali ya Norway.

Kati ya shughuli muhimu zilizopangwa ili kutekeleza malengo ya mradi na kuimarisha uhusiano na wakulima, watafiti na washauri wa wakulima ni kufanya warsha zenye madhumuni yafuatayo:

1. Kuwajumuisha watafiti, wakulima na washauri wa kilimo ili kudadisi kuhusu mambo muhimu yanayohitaji kushirikishwa pande zote kwa lengo la kufanikisha kilimo na ufugaji
2. Kuchambua na kuainisha matatizo yanayowakabili wakulima wadogowadogo
3. Kupanga ili kutambua mambo gani yapewe uzito au kipaumbele
4. Kushiriki katika kupeana uzoefu wa maeneo muhimu ya kilimo na mifugo.

Chapisho hili linawasilisha mwenendo wa warsha ya nane ya wakulima wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuhusu **Uendelezaji wa Vikundi vya Wakulima** iliyofanyika ukumbi wa Allamano wa Vijana wa Kikatoliki, Makambako, Njombe, 7-9, Juni 2004. Mwenendo wa warsha umechapishwa na kutolewa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

*L. D. B. Kinabo*
*Mratibu wa Mradi*

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ARDA | Chama cha Kilimo na Maendeleo Vijijini, Rukwa |
| IRDTF | Shirika la Ufadhili wa Maendeleo Vijijini, Ileje |
| MAFS | Wizara ya Kilimo na Chakula |
| MVIWAI | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Ileje |
| MVIWAMBO | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Mbozi |
| MVIWATA | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania |
| NGO | Shirika lisilo la Kiserikali |
| NLH | Chuo Kikuu cha Kilimo cha Norway |
| SUA | Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo |
| TARP II | Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo Awamu ya Pili |
| TGNP | Mtandao wa Jinsia Tanzania |
| UNDP | (Shirika la Umoja wa Mataifa la Mipango ya Maendeleo |

# 1.0 UTANGULIZI

Warsha ya Uendelezaji wa Vikundi vya Maendeleo ya Wakulima iliyofanyika ni kati ya mafunzo ambayo hutolewa na mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la kaya (TARP II SUA). Mradi huu unatekelezwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula (MAFS) pamoja na Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo (NLH). Washiriki katika warsha walitoka mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma. Jumla ya washiriki wa warsha hii walikuwa 29 ikijumuisha wakulima 14, wataalamu wa ugani 4, watafiti 9 na taasisi zisizo za serikali 2. Orodha ya washiriki imeambatishwa katika kiambatisho Na. 1. Warsha ilifanyika kuanzia tarehe 7 hadi tarehe 9 Juni 2004 katika ukumbi wa Allamano wa Vijana wa Kikatoliki, Makambako, Njombe. Warsha hii iliandamana na utoaji zawadi kwa wakulima, wagani, na watafiti bora katika kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

## 1.1 Madhumuni ya warsha

Madhumuni ya warsha yalikuwa ni;

- Kuwawezesha washiriki kupata mbinu mbalimbali za uongozi na uendeshaji wa vikundi.
- Kuwawezesha waashiriki kujifunza jinsi ya kuandaa mipango ya maendeleo ya vikundi.

## 1.2 Ufafanuzi wa Maneno

Ili kuwawezesha washiriki kuwa na uelewa mmoja katika warsha, ufafanuzi wa maneno yaliyotumika katika warsha ulifanyika. Ufafanuzi wa maneno yaliyotumika ni:

**Kikundi:** Ni ushirikiano wa watu walioamua kwa hiari yao wenyewe kujiunga pamoja kwa nia ya kutatua matatizo yao yanayowakabili.

**Mtandao:** Ni muungano wa vikundi mbalimbali katika ngazi mbalimbali; kwa mfano kijiji, kata, tarafa, wilaya, mikoa na taifa.

**Katiba:** Ni desturi, kawaida, taratibu zilizo za lazima ambazo zinatumika kama mwongozo katika uendeshaji wa shughuli za kikundi.

**Uongozi:** Ni utaratibu unaowekwa ili kusaidia, kusimamia na kuratibu shughuli za kikundi siku kwa siku.

**Migogoro/migongano katika vikundi:** Migogoro ni hali ambayo hujitokeza pale pande mbili au zaidi zinapoona kwamba nia ya kupata madaraka au mali, kushiriki katika kutoa maamuzi dhidi ya maslahi ya jamii na hayawezi kufikiwa kwa wakati au zinapotambua tofauti katika mahitaji, utashi, na imani

**Mtaalamu wa ugani:** Ni mtumishi anayetoa ushauri wa kitaalamu wa aina mbalimbali kwa jamii ili utumiwe katika maisha ya kila siku. Watumishi kama afisa maendeleo ya jamii, kilimo, afya, mifugo huitwa maafisa ugani.

**NGO:** Ni taasisi isiyo ya kiserikali, inayofanya kazi kufuata taratibu iliyojiwekea ambazo zinawiana na sera za nchi, yenye lengo la kuwezesha jamii kuboresha hali ya maisha.

**Mtafiti:** Ni mtu anayefanya uchambuzi wa kina katika kubaini matatizo au vikwazo vilivyopo katika jamii vya uendeshaji wa maisha ya mwanadamu na kubuni au kupendekeza utatuzi wake.

## 1.3 Matarajio na Hofu ya Warsha

Ili kuelewa na kuainisha mahitaji ya wana-warsha, kila mshiriki alipata fursa ya kueleza matarajio yake pamoja na hofu ambazo zingekuwa kikwazo katika warsha. Majumuisho ya matarajio na hofu yalikuwa;

**Matarajio**

- Kupata mafunzo na kuwaeleza wenzangu
- Kupata uhalisi wa matatizo ya vikundi vya wakulima
- Kupata maoni kutoka kwa wakulima, waghani juu ya hali ya kiuchumi
- Kujua mbinu endelevu ya chakula na pato la kaya
- Kupata elimu juu ya kilimo cha kisasa na ufugaji bora
- Kujifunza mbinu za uundaji, uongozi na uhamasishaji wa vikundi.
- Kubadilishana uzoefu juu ya shughuli za vikundi toka kwa wakulima na wataalamu.
- Kupata taarifa ya maendeleo ya utafiti

**Hofu**

Washiriki walikuwa na hofu kuhusu warsha kama ifuatavyo:

- Hali ya afya sababu ya shida ya maji na baridi
- Muda hautatosha
- Wana-warsha kutokusaidiana kama mtu haelewi
- Kutokumaliza warsha
- Itawezekana kufikisha malengo ya warsha?

## 1.4 Mbinu zilizotumika

Mbinu ya ushirikishwaji ilitumika ili kumwezesha kila mshiriki kupata nafasi ya kuchangia kwa uhuru zaidi. Njia zilizotumika ni pamoja na :

- Majadiliano katika vikundi ambapo vikundi viligawanywa wakulima peke yao, watumishi wa ugani, na vya wanawake walio wengi
- Visa mikasa
- Vibwagizo
- Michezo kama kuzama boti, kuandika jina juu ya paji la uso
- Hadithi
- Michoro ya chapati katika kutambulishana

Njia hizo zote ziliwezesha washiriki kuweza kulinganisha mazingira na hali halisi ya maendeleo ya vikundi na jinsi vinavyoweza kujikwamua na kuwa endelevu

### 1.4.1 Majadiliano katika vikundi

Washiriki walifanya kazi za vikundi ili kupata nafasi ya kubadilishana uzoefu kutoka maeneo mbalimbali yanayowakilishwa kwenye warsha. Washiriki kupitia vikundi waliweza kutoa uzoefu wao kuhusu maendeleo ya vikundi wakichambua uwezo na udhaifu wa vikundi, na hatua zinazochukuliwa ili kufanya vikundi kuwa endelevu.

### 1.4.2 Taarifa za vikundi

Washiriki waliweza kujadili na kutoa changamoto mbalimbali kwa kurejea maeneo wanayotoka kama ifuatavyo:

| UWEZO/NGUVU | UDHAIFU | UTATUZI |
|---|---|---|
| • Vikundi vilivyoanzishwa kwa shughuli za maendeleo vina uwezo wa kujiendesha na kujiongoza kwa sababu vina mwelekeo wa kisheria (katiba).<br>• Vikundi vipo na vinafanya kazi za utafiti na uchumi.<br>• Vikundi vinajiwekea | • Wanakikundi wengi wanajiunga kwenye vikundi wakiwa na mawazo tegemezi hasa ya kupata misaada<br>• Vikundi havina usajili wa kudumu<br>• Vikundi vingi havina mtaji wa kutosha<br>• Vikundi vingi | • Kushauri vikundi rejea ya shughuli mbali mbali na kutumia katiba kama mwongozo.<br>• Vikundi kurejea malengo yaliyowekwa na kuandaa yanayokubalika kama hatua ya kuvifanya kuwa endelevu.<br>• Vikundi vijenge tabia ya kujiwekea akiba ili kuondokana na |

| | | |
|---|---|---|
| akiba benki.<br>• Kurutubisha udongo na kupata mazao mengi.<br>• Ushirikiano wa wanavikundi katika shughuli mbalimbali<br>• Kuhamasisha vikundi kupitaia vikao | vina malengo ya muda mfupi<br>• Vikundi vingi vina mitandao dhaifu<br>• Elimu duni ya uendeshaji wa vikundi<br>• Vikundi havifahamu sera mpya ya vikundi<br>• Vikundi vingi havina malengo yanayoeleweka<br>• Wataalamu wachache<br>• Mbinu tofauti kwa baadhi ya taasisi mbalimbali katika kuwaendea walengwa | tabia tegemezi ikiwa ni pamoja na wanavikundi wenyewe kujiwekea akiba zao binafsi.<br>• Vikundi vinatakiwa kupatiwa elimu ya uendeshaji wa vikundi pia kushirikisha sekta mbalimbali za umma.<br>• Vikundi viwe na uongozi imara wenye msimamo katika kutetea maslahi yao. |

## 2.0 UMUHIMU WA VIKUNDI NA UUNDAJI WAKE

Suala la kuwepo kwa vikundi ni la msingi kwa kuwa linawezesha wana-jamii kuweza kuunganisha nguvu zao kwa pamoja kwa ajili ya kufanikisha au kutatua matatizo yanayowakabili. Uzoefu umeonesha kuwa vikundi vingi vimeanzishwa kwa lengo la kufanya shughuli pamoja. Baadhi wameshamiri na kufanikiwa kufikia malengo yake. Aidha baadhi ya vikundi vimezorota na hatimaye kufa muda mfupi tu baada ya kuanzishwa. Watu wanaposhirikiana kwa pamoja, hufanya mambo mengi kwa wakati mmoja na hatimaye kwa kufanya kazi pamoja wanafikia malengo yao na kupata maendeleo ya haraka. Kikundi kinakuwepo endapo kutakuwa na mambo makuu yafuatayo:

- Watu
- Uhusiano mzuri
- Hiari

Umuhimu wa kujiunga kwenye kikundi ni:

- Kutatua matatizo au haja zinazowakabili
- Kufanya kazi kwa pamoja
- Kuongeza ushirikiano
- Kuharakisha utendaji wa kazi
- Kurahisisha huduma na kutambulika
- Kujifunza kwa wengine
- Kuongeza mapato na kugawana faida

**Muhimu**

Inabidi kikundi kuwa na malengo na mpangilio wa shughuli mbalimbali za kiuchumi au za huduma.

## 2.1 Kuunda Kikundi

Wazo la kuunda kikundi hutokana na mtu mmoja au watu wachache wakati kuna tatizo linalohitajika kutatuliwa. Wakati mwingine watu wenye mahitaji tofauti na mitizamo tofauti au kwa kuwa na majadiliano juu ya jambo linalowakabili huamua kuunda kikundi. Kikundi kinachoundwa kinaweza kuwa cha:

- Uchumi
- Huduma

Uzoefu umeonesha kuwa vikundi vingi hufa baada ya kuanza kwa sababu wanakikundi huamua kujiunga bila kutambua malengo ya kuwa kwenye kikundi. Hali hii hupelekea wanachama kutopata matakwa yao. Wakati mwingine vikundi huanzishwa na miradi moja kwa moja bila matayarisho na uelewa wa mazingira na mawazo ya wakulima. Ikumbukwe kwamba kuanzisha kikundi ni kitu cha hiari na hufanywa na watu wenyewe na siyo pandikizo kutoka nje. Vikundi vingi vinavyoanza kwa pandikizo la nje mara nyingi uwajibikaji unakosekana na utegemezi uliokithiri huongezeka hali ambayo hupelekea vikundi kuwa na shughuli zisizokuwa endelevu.

## 2.2 Mambo muhimu ya kuangalia katika kuunda kikundi

Ili kikundi kiweze kuundwa na kujiletea mafanikio ni vyema wale wanaounda kikundi wawe na malengo ya aina moja na yanayokubalika na kuzingatiwa na wanakikundi wote. Wanakikundi wakiyafahamu watakuwa na ari ya kuyatekeleza ili yafanikiwe. Kutokana na hali hiyo masuala yafuatayo budi yaangaliwe:

- Wanakikundi wanatakiwa kutojiunga kwenye kikundi kabla hawajapata jibu la kwa nini, na kama kweli kikundi kinahitajika.
- Kikundi kiundwe kama kweli kinahitajika

- Kikundi kinatakiwa kuundwa na watu wanaoona umuhimu, na kwa kuzingatia mazingira yaliyopo na kwa nia ya kutatua tatizo kwa kuwa kwenye kikundi

Kikundi kinachoundwa kwa kulazimishwa mara nyingi hakipati mafanikio endelevu. Ili kupata kikundi kizuri sharti kuchambua maswali haya yafuatayo kuhusu wahusika:

- Je, wana uzoefu wa kufanya kazi pamoja?
- Je, ni sifa na tabia gani ambazo mwanakikundi anapaswa kuwa nazo?
- Je, wanaishi karibu au mbalimbali?
- Je, wangependa kufanya kazi pamoja?
- Je, upo utaalamu wa kutosha wa kuziendesha kazi za kikundi kwa mafanikio?
- Je, wanamudu kiasi gani kupata mahitaji ya shughuli wanayotaka kuanzisha?
- Kila mwanachama achangie kiasi gani?
- Kuna haja ya kutafuta nguvu toka nje ya kikundi?

**Angalizo**

*Maswali kama haya yanachangia kujenga msingi wa kupata aina ya wanakikundi watakaokubalika kuunda na kukiendesha kikundi. Katika kuanzisha kikundi, hakuna idadi inayopendekezwa bali hutegemeana na maamuzi ya wananakikundi na pia kutegemeana na shughuli inayofanyika*

### 2.3 Ukuaji wa Kikundi

Kwa kawaida ukuaji wa vikundi unafuata mtiririko ufuatao:

**Hatua ya 1**

- Mtu mmoja au kikundi kuwa na wazo la kutatua tatizo fulani

- Kunakuwa na nia ya kutatua tatizo fulani
- Mwamko na shauku kubwa ya kuhusu lengo la kikundi
- Mawasiliano ni kwa mdomo zaidi kuliko maandishi

**Hatua ya 2**

- Hufikiwa pale inapotokea migongano ya mawazo mbalimbali
- Kupungua mshikamano
- Waanzilishi wa kikundi wanaweza kuamua kuondoka hivyo pengo kubwa kutokea
- Utegemezi uliokithiri

**Hatua ya 3**

- Haja ya kuimarisha mawasiliano hujitokeza
- Umuhimu wa kuwa na vikao vya mara kwa mara hujitokeza
- Muundo wa uongozi kueleweka
- Taratibu sera mbalimbali kuandaliwa

**Hatua ya 4**

- Ni wakati wa kujiimarisha
- Maandalizi ya utendaji hupewa kipaumbele
- Taratibu za kiutendaji kuimarishwa
- Ongezeko la moyo wa kujitolea

Kutokana na uzoefu kutoka kwa washiriki ulidhihirisha kuwa vikundi vilivyohudhuria warsha karibu vyote viko katika kipindi cha mpito. Vikundi vichache vilikuwa kati ya hatua ya kwanza na ya pili.

## 2.4 Uundaji wa Mtandao

Mtandao ni muungano wa vikundi mbalimbali katika ngazi mbalimbali mfano kijiji, kata, tarafa, wilaya, mikoa na taifa. Mtandao katika maeneo ya Nyanda za Juu Kusini ni kama vile Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Mbozi (MVIWAMBO), Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Ileje (MVIWAI), Mtandao

wa jinsia, n.k. Mitandao ya kitaifa ni kama vile MVIWATA, Mtandao wa jinsia (TGNP), na mingineyo.

Ni vema kutambua kuwa **kikundi kinahusu watu wenye tatizo, nia na lengo moja** na **mtandao unahusu vikundi vilivyoungana kwa lengo la mawasiliano; kama vile, kwa lengo la kutafuta masoko, au kubadilishana uzoefu juu ya jambo fulani.** Ili kujenga mtandao imara ni lazima:

- Vikundi imara ndiyo viunde mtandao
- Kuwepo na michango toka kwa wanavikundi wanaounda mtandao
- Kuwepo kwa wawakilishi katika mtandao
- Kuchagua viongozi wa mtandao

Mtandao unaweza kufananishwa na nyumba ya buibui ambayo huanza kujenga nyumba yake kwa kuweka nguzo pande zote na kisha huweka njia za kutambaa katika kila kona kupitia njia zake zote.

# 3.0 MISINGI YA VIKUNDI BORA

Ili kikundi kiweze kuwa imara hufuatiwa na utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za kikundi na jinsi kila mwanakikundi anavyotekeleza wajibu wake katika kukiendeleza kikundi.

**Uongozi**

Katika kuweka misingi imara ya maendeleo ya vikundi mfumo wa uongozi huhitajika ili kikundi kipate ufanisi katika:

- Kupanga na kuainisha malengo
- Kuwaunganisha wanakikundi
- Kuratibu kazi za kikundi
- Kusimamia mali za kikundi

Uongozi unahusisha viongozi wote wa kikundi ambao ni mwenyekiti, katibu, mweka hazina, na kamati ya kikundi. Kwa hiyo uongozi unatakiwa kudumisha upendo, mshikamano, na kusimamia mambo yote yaliyotajwa. Uongozi mzuri hutoa haki sawa ya ushiriki katika kikundi kwa viongozi na wanakikundi wake.

Mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa katika uongozi ni pamoja na:

- Kusikiliza maoni ya wanakikundi
- Kujadili kwa pamoja mambo mbalimbali na kufikia maamuzi kwa pamoja kama vile mipango ya kikundi
- Kuaminiana na kuheshimiana

Ili kuwepo na ufanisi mzuri suala la kuzingatia ni kuwa na viongozi wenye sifa nzuri

# 4.0 TABIA MBALIMBALI ZA WATU KATIKA VIKUNDI

## 4.1 Maana ya Tabia

Washiriki walitoa ufafanuzi kuwa tabia ni mwenendo au hali fulani ambayo mtu anaifanya kufuatia mazingira yanayomzunguka bila kujitambua au kuelewa kinachofanyika kwa nia ya kuboresha au kuharibu. Zipo tabia nzuri na tabia mbaya ambazo huweza kujionesha mbele ya macho ya watu na hivyo kupata nafasi ya kuzitoa kasoro au kuzipa umaarufu fulani kufuatia taratibu zilizowekwa na jamii. Tabia hutegemeana sana na malezi, mazingira, kiwango cha elimu, mila na desturi zilizopo katika jamii husika.

Tabia za watu zinaweza kuleta mafanikio au kushindwa kufikia malengo yaliyowekwa iwapo hakuna udhibiti. Watu wanapokuwa pamoja, kila mmoja hutofautiana na mwenzake. Tabia nzuri huchangia kuleta umoja, ushirikiano, usalama, upendo, uaminifu, utulivu, na uangalifu. Ili kuweza kudhibiti tabia mbovu ndani ya kikundi inabidi kuzitambua na kuzichukulia hatua ili kudumisha umoja/mshikamano. Uzoefu umeonesha kuwa kila mtu anaangukia kwenye tabia haribifu kutokana na hali ya kurithishwa au na mila na desturi zilizopo. Hata hivyo tabia hizi zinaweza kubadilishwa kwa kujifunza na mazingira yaliyopo. Kwa hiyo tabia siyo kitu cha kudumu.

## 4.2. Aina za Tabia za Watu katika Jamii

Washiriki walipata nafasi ya kuchambua tabia mbalimbali zilizopo katika jamii. Tabia hizi ni pamoja na tabia ya kitoto; kujikweza; ukorofi; ubinafsi.
Tabia hizi zinaweza kufananishwa na wanyama mbalimbali kama ifuatavyo:

| Aina ya mnyama | Tabia yake |
|---|---|
| Punda | Ana akili nyingi; Ni rafiki wa wanadamu; Ni mkaidi; Ni mvumilivu. |
| Simba | Ni jeuri; Ana maonezi; Ana hasira; Ni mkali |
| Sungura | Ni mjanja; Ni mwerevu; Ni mkwepaji; Hutoroka pale anapoona kuna shida; Haeleweki |
| Paka | Anapenda kubembelezwa; Ana usiri; Anataka kuhurumiwa daima. |
| Tausi | Anapenda kutambuliwa kwa uzuri wake; Ana majivuno; Ni msafi; Ana kimbelembele |
| Kinyonga | Kigeugeu; Huchukuwa muda kuamua |
| Tembo | Ana kiburi; Siyo mwoga |

Washiriki walibaini kuwa aina ya tabia zote zilizotajwa zinapatikana katika maeneo mbali mbali na zipo kwa wanakikundi ndani ya vikundi na kila mwanakikundi ana tabia ambayo inafanana na tabia iliyotajwa hapo juu walau moja na wengine wanaweza wakahusika na tabia zote.

Uzoefu umejitokeza kuwa zipo tabia ambazo zinaweza kurekebishwa ila itategemea mazingira mtu atokayo; maeneo ya kazi; na hata kupitia vikundi mbalimbali vyenye katiba au sheria za udhibiti mzuri zinasaidia kurekebisha baadhi ya tabia za wahusika.

## 4.3 Migogoro/Migongano

Washiriki waliweza kujadiliana na kubainisha aina ya migogro/migongano, jinsi inavyotokea katika vikundi vyao, na namna migogoro inavyosuluhishwa pale inapotokea. Majumuisho ya mawasilisho ya majadiliano ya wana-warsha yalikuwa kama ifuatavyo:

| Migogoro / Migongano | Utatuzi |
|---|---|
| • Migongano ya kiuchumi, tofauti ya vipato kwa wanakikundi, na kufuja mali ya kikundi (hasa viongozi)<br>• Migongano ya kijamii ambapo ubinafsi na ukorofi kati ya wanajamii/ wanakikundi unatawala<br>• Migongano ya kielimu ndani ya kikundi mfano: watumishi/wakulima<br>• Migogoro ya maamuzi katika utekelezaji yaani wanakikundi kutofika na kutekeleza maazimio yaliyoamuliwa<br>• Migongano/migogoro wakati wa kusomewa taarifa ya mapato ya kikundi baadhi ya wanakikundi kutokubaliana na mahesabu yaliyosomwa<br>• Migongano/migogoro wakati wa uchaguzi wa viongozi wa kikundi hutokea mgawanyiko kwa wanakikundi, baadhi hutoa vivutio kwa wanakikundi kwa lengo la kuchaguliwa ijapokuwa hawana sifa, na upendeleo katika uchaguzi, anayesimamia | • Kutumia vikao<br>• Kubadili mfumo wa uongozi<br>• Walengwa kushika uongozi badala ya watumishi<br>• Kutoa taarifa za maendeleo ya kikundi za mara kwa mara.<br>• Tatizo linapotokea ni budi lipelekwe kwenye kamati ya nidhamu ya kikundi ili litafutiwe ufumbuzi ulio wa haki<br>• Kuonywa mara ya kwanza na endapo atarudia tena kufukuzwa uanachama<br>• Faini hutolewa kwa kosa dogo.<br>• Kukaa pamoja katika kikao cha kikundi na kutafuta suluhisho pamoja na ufumbuzi wa matatizo<br>• Kuwa na katiba inayoeleweka na inayotumika |

| | |
|---|---|
| uchaguzi kumpitisha anayemtaka<br>• Baadhi ya wanakikundi kuingilia kazi za viongozi wa kikundi<br>• Baadhi ya wanakikundi kutoshiriki kikamilifu katika shughuli za kikundi na kuanzisha majungu kwa kutafuta haki<br>• Baadhi ya viongozi wa vikundi kutumia madaraka vibaya na kufanyia maamuzi yao wenyewe bila kushirikisha wanakikundi. | |

### 4.4 Chimbuko la Migogoro katika Vikundi

Migogoro hujitokeza pale pande mbili au zaidi zinapoona kwamba nia ya kupata madaraka au mali, kushiriki katika kutoa maamuzi dhidi ya maslahi ya jamii na hayawezi kufikiwa kwa wakati au zinapotambua tofauti katika mahitaji, utashi, na imani. Hapa mvutano huanza kujitokeza na mvutano huu usipotatuliwa mapema hukua na kuzaa mgogoro.

Kwa maneno mengine inapotokea kundi moja au sehemu ya watu katika jamii wananyimwa nafasi katika kushiriki, kusikilizwa katika maamuzi yanayoigusa jamii nzima na kuona kuwa wananyimwa haki na hivyo kudai hali iboreshwe zaidi. Kwa hiyo, migogoro mingi tuliyo nayo au tuliyowahi kuiona na kusikia ni matokeo ya hatua za MAENDELEO katika jamii.
Migogoro inaweza kuibuka iwapo kuna:

- Ukiukwaji wa taratibu, matumizi ya mabavu katika kuendesha/kutoa maamuzi ya shughuli za jamii

- Tabaka za kikabila au kiitikadi
- Tofauti za kiuwezo katika nyanja za elimu na umiliki wa rasilimali

Hata hivyo ikumbukwe kuwa ipo migogoro pia ambayo huwezi kuitambua au isiyojitokeza. Hii ni pamoja na hofu; kutojiamini; tofauti ya uwezo; na kutengwa na jamii. Uzoefu umeonesha kwamba, migogoro isiyojitokeza hasa ndiyo iliyopo katika vikundi vilivyo vingi na imeleta madhara makubwa ndani ya kikundi inapotokea. Kwa hali halisi maeneo yanayoongoza kusababisha migogoro ni pamoja na:

- Masuala ya uongozi
- Ugawanyaji wa rasilimali
- Malengo tofauti
- Tofauti za mvuto/utashi na raghba

Sababu nyingine zinazochangia kuwepo kwa migogoro ni pamoja na:

- Ushirikishwaji hafifu katika kupanga na kutekeleza shughuli za kikundi na kijamii
- Mbinu dhaifu juu ya utatuzi wa migogoro
- Mawasiliano duni hasa katika masuala yanayogusa vikundi na jamii kwa ujumla
- Tabia ya kutokuwa wakweli na wazi ambapo hupelekea kutoaminiana
- Mahusiano ambayo hayana uwiano baina ya wadau katika shughuli za kijamii

Uchambuzi uliofanywa na washiriki, umeonesha kwamba, zipo athari za kuwepo kwa migogoro ambayo husababisha:

- Kusambaratika kwa umoja
- Huduma za maendeleo kuathirika
- Kufa au kudhoofu kwa uhusiano
- Kujenga zaidi uhasama

Ikumbukwe kuwa migogoro ni sehemu ya kujiletea maendeleo. Hivyo basi, kuna faida zake ambazo ni:

- Kutoa haki sawa za umiliki na uongozi
- Kudumisha mshikamano

Ni vema kufanya usuluhishi wa migogoro mara itokeapo bila kuchelewa. Ili kuweza kufanya suluhisho la migogoro, inabidi kuwe na mikakati ifuatayo:

- Suluhisho kwa kutumia nguvu
- Usuluhishi
- Maafikiano
- Kutumia sheria
- Kukwepa

# 5.0 KATIBA YA KIKUNDI

Katiba huhitajika sana katika kikundi ili itumike kama mwongozo. Katiba hutengenezwa kulingana na mazingira na malengo ya kikundi. Katiba inayotumika ipasavyo na wanakikundi inasaidia kikundi kufikia malengo yaliyowekwa. Kiambatisho Na. 2 kinaonesha hali ya malengo yaliyowekwa na vikundi mbalimbali.

Katiba ni desturi, kawaida, taratibu zilizo za lazima ambazo zinatumika kama mwongozo katika uendeshaji wa shughuli. Katiba husaidia kuratibu:

- Mwenendo wa viongozi na wanakikundi
- Kazi za kikundi
- Mali ya kikundi
- Haki na wajibu
- Sifa za anayeomba uanachama.

Wakati wa kutengeneza katiba ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo:

- Malengo ambayo kikundi kinatarajia kuyafikia
- Sifa zitakazokubalika ili kujiunga na kikundi, masharti ya kujiunga na viingilio.
- Aina ya uongozi wa kikundi, sifa, na muda wa uongozi
- Jinsi ya kuendesha kazi za kikundi
- Ugawaji wa mapato ya kikundi
- Mipaka na maadili ya uongozi

## 6.0 MAPENDEKEZO NAMNA YA KUBORESHA VIKUNDI

i. Kutokana na maelezo ya washiriki ilibainika kuwa wakulima watafiti na baadhi ya vikundi hawapati huduma za ugani kadri ya matakwa yao, hali ambayo inasababisha vikundi kukosa baadhi ya huduma na ushauri kutoka kwa maafisa ugani. Wanawarsha walipendekeza kwamba vikundi vinatakiwa kutembelewa mara kwa mara na wataalamu ili vielekezwe jinsi ya kuandaa malengo endelevu ya vikundi, uandaaji wa katiba, na jinsi ya kusuluhisha migongano / migogoro katika vikundi.

ii. Vikundi vya wakulima vinavyofanya utafiti na TARP II SUA vinatakiwa kuwezeshwa jinsi ya kubuni miradi mingine baada ya kufanya utafiti wa muda mrefu.

iii. Washiriki walibaini kuwa baadhi ya vikundi vinavyofanya kazi na TARP II SUA bado havijafikia hatua ya kujitegemea; hali ambayo inaweza kupelekea vikundi vingi kutokuendelea baada ya mradi kuisha. Ilipendekezwa kuwa TARP II SUA kuwa na mikakati ya makusudi ya jinsi ya kuviandaa vikundi kujitegemea na kuwa endelevu ili kuweza kupata matokeo halisi ya mradi baada ya mradi kufikia mwisho.

iv. Ilidhihirika kuwa bado kuna utegemezi uliokithiri wa wanavikundi hali inayopelekea wanakikundi kutojituma ili kujenga vikundi vyao. Ilipendekezwa kuwa wakulima wenyewe wanatakiwa kujitoa na kuwa na moyo wa kujituma katika kuendeleza vikundi vyao.

v. Kutokana na uzoefu wa washiriki imeonekana kuwa shughuli nyingi za miradi huwa haziwahusishi viongozi wa ngazi mbalimbali kama dini na serikali. Wito ulitolewa

na washiriki kuwa wanatakiwa kutambulisha shughuli za kila kikundi katika serikali na taasisi nyinginezo na pia washirikishwe katika kuhamasisha uendelezaji wa vikundi.

vi. Imeonekana kuwa vikundi vingi vimeanza bila kupata elimu ya kina ya kuhusu vikundi. Ilipendekezwa kuwa elimu ya vikundi itolewe zaidi katika ngazi ya kijiji ili watu wengi zaidi wapate elimu hii muhimu.

vii. TARP II SUA ifanye utaratibu wa kutoa mafunzo kwa wakulima wachache watakaokuwa wanatoa elimu ili kupunguza matatizo na malalamiko ya wakulima kuhusu kukosa huduma ya wataalamu. Ikiwezekana TARP II SUA ihusishe taasisi zisizo za kiserikali ili ziweze kuchukua jukumu hilo mara mradi utakapokamilisha muda wake.

# 7.0 HITIMISHO

Katika kuhitimisha warsha washiriki waliandaa mipango ya utekelezaji wa shughuli zao zitakazohusu uendelezaji wa vikundi (Kiambatisho Na. 3) na pia walifanya tathmini ya mwenendo wa warsha kabla warsha haijafungwa.

## 7.1 Mipango ya Utekelezaji

Washiriki waliandaa mipango ya utekelezaji wa kazi ambazo zinalenga kuboresha vikundi vyao. Mipango hii ni matokeo ya mafunzo ambayo washiriki waliweza kutambua matatizo/mapungufu ya vikundi vyao na hivyo kuonesha nia ya kutaka kufanya maboresho. Mipango ya utekelezaji wa kazi uliandaliwa na kila kikundi ili kurahisisha ufuatiliaji wa shughuli kama zilivyopangwa. Kiambatisho Na. 3 kinatoa maelezo ya kina katika mipango ya kazi.

## 7.2 Tathmini ya Warsha

Tathmini ya mchakato mzima wa warsha ilifanywa na washiriki nao walikiri wazi kuwa warsha iliwaongezea kiwango cha upeo na ufani wa uendelezaji wa vikundi vyao. Aidha walibainisha kuwa malengo ya warsha yalifikiwa na mbinu za uwezeshaji ziliwawezesha kuelewa vizuri mada zilizokuwa zinatolewa.

Washiriki walipendekeza mafunzo kama haya ya uimarishaji vikundi yatolewe kwa vikundi vingine ili vipate elimu hii muhimu kwa maendeleo ya vikundi.

## 7.3 Kufunga Warsha

Warsha ilifungwa rasmi na Afisa Tawala Wilaya ya Njombe, Bi P. Wiketye kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya. Shughuli hii iliambatana na kutoa zawadi kwa Wakulima, Wagani na Watafiti

mahiri katika utekelezaji wa mradi kutoka kanda ya Nyanda za Juu Kusini na SUA. Mgeni rasmi alisisitiza juu ya mipango ya kazi iliyoandaliwa kuwa ni hatua nzuri na hivyo kila mmoja anatakiwa kwenda kuifanyia kazi kwa ajili ya maendeleo ya kikundi chake kwa utaratibu kama ulivyoandaliwa katika kiambatisho namba 3.

# 8.0 VIAMBATISHO

## 8.1 Kiambatanisho Na. 1: Orodha ya Washiriki wa Warsha

| Na | Jina | Jinsi | Kazi | Kijiji | Kata | Anuani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Avelina Mbunda | Ke | Mkulima | Kitanda | Utili | S.L.P. 50, Mbinga, Ruvuma |
| 2. | Mwanaidi Ismaili | Ke | Mkulima | Itope | Busale | S.L.P. 201, Kyela, Mbeya |
| 3. | Lukanus Ponela | Me | Mkulima | Mlete | Tanga | S.L.P. 59 Songea, Ruvuma |
| 4. | Maimuna Hamza | Ke | Mkulima | Mgombasi | Mgombasi | S.L.P. 82, Namtumbo, Ruvuma |
| 5. | John Mwambuchi | Me | Mkulima | Ibumila | Igongolo | S.L.P. 323, Njombe, Iringa |
| 6. | Julius Ntalyaga | Me | Mkulima | Kankwale | Senga | S.L.P. 468, Sumbawanga, Rukwa |
| 7. | Selina Omari | Ke | Mkulima | Matai | Matai | S.L.P. 232, c/o N. Ngusi Sumbawanga |
| 8. | Filipo Y. Mapunda | Me | Mkulima | Kitanda | Utili | S.L.P. 232, Mbinga, Ruvuma |
| 9. | Falazia M. Bilaury | Ke | Mkulima | Katonto | Kaengesa | S.L.P. 34 Sumbawanga, Rukwa |
| 10. | Daina G. Mangula | Ke | Mkulima | Ibumila | Igongolo | S.L.P. 323, Njombe, Iringa |
| 11. | Veronika Samlongo | Ke | Mkulima | Kisilo | Uwemba | S.L.P. 229, Njombe, Iringa |
| 12. | Crispin Nandi | Me | Mkulima | Matai B | Matai | S.L.P. 232, c/o N. Ngusi Sumbawanga |
| 13. | Enitha Kisota | Ke | Mkulima | Matebete | Chimala | S.L.P. 126, Mbarali, Mbeya |
| 14. | John Mwandemele | Me | Mkulima | Kikusya | Busale | S.L.P. 150, Kyela, Mbeya |
| 15. | Martha Kashu | Ke | Mkulima | Matebete | Chimala | S.L.P. 126, |

| Na | Jina | Jinsi | Kazi | Kijiji | Kata | Anuani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Mbarali, Mbeya |
| 16. | Patrick Mwabena | Me | Mkulima | Kisilo | Uwemba | S.L.P. 229, Njombe, Iringa |
| 17. | Nuhu Y. Mohamed | Me | Mghani | Ibumila | Igongolo | S.L.P. 168, Njombe, Iringa |
| 18. | Nictor Y. Ngusi | Me | Mghani | Matai | Matai | S.L.P. 232, Sumbawanga, Rukwa |
| 19. | Regina E. Kihwele | Ke | Mghani | Ichenga, FTC | Uwemba | S.L.P. 58, Njombe, Iringa |
| 20. | Michael Mwampaja | Me | Mghani | Kikusya | Busale | S.L.P. 188, Kyela, Mbeya |
| 21. | Savelina Katunzi | Ke | ARDA | Mazwi | Sumbawanga | S.L.P. 232, Sumbawanga, Rukwa |
| 22. | Peter A. Kindimba | Me | Ileje RDTF | Msia | Chitete | S.L.P. 160, Ileje, Mbeya |
| 23. | Isumaili Ole Kisangas | Me | Emanyata | Matebete | Chimala | S.L.P. 126, Mbarali, Mbeya |
| 24. | Sophia Swai | Ke | Mtafiti | ARI-Uyole | Uyole | S.L.P. 400, Mbeya |
| 25. | Ndabhemeye Mulengera | Me | Mtafiti | ARI-Uyole | Uyole | S.L.P. 400, Mbeya |
| 26. | Lameck Makoye | Me | Mtafiti | ARI-Uyole | Uyole | S.L.P. 400, Mbeya |
| 27. | Faustin P. Lekule | Me | Mtafiti | SUA | Mbuyuni | S.L.P. 3004 Morogoro |
| 28 | Emmanuel K. Batamuzi | Me | Mtafiti | SUA | Mbuyuni | S.L.P. 3020 Morogoro |
| 29 | Akwilini J. P. Tarimo | Me | Mtafiti | SUA | Mbuyuni | S.L.P. 3005 Morogoro |
| 30 | Elimpaa D. Y. Kiranga | Me | Mtafiti | ARI-Uyole | Uyole | S.L.P. 400, Mbeya |
| 31 | Joyce G. Lyimo-Macha | Ke | Mtafiti | SUA | Mbuyuni | S.L.P. 3044, Morogoro |
| 32. | Fausta Valery | Ke | Mwezeshaji | MBEYA | Mbeya | S.L.P.2030, Mbeya |

## 8.2 Kiambatisho Na. 2: Hali na Malengo ya Vikundi

| JINA LA KIKUNDI (Kilipoanza) | KIJIJI | WILAYA | LENGO LA KIKUNDI | UWEZO | UDHAIFU |
|---|---|---|---|---|---|
| Naretisho (2002) | Matebete | Mbarali | Kuinua kipato cha akina mama ili kujikimu na maisha kwa kufanya shughuli mbalimbali za mikono na ufugaji | Kushona vitu mbalimbali kama vile mikufu na mikanda, Baadhi ya wanakikundi wana baiskeli ambazo hutumika kusafirishia bidhaa hata za kikundi kwenye eneo la kuuzia | • Kikundi bado kichanga<br>• Umbali na soko la kuuzia bidhaa pamoja na maziwa<br>• Kukosa soko kamili la kuuzia bidhaa zinazozalishwa |
| Motomoto | Mgombasi | Songea | Kilimo cha tumbaku na mpunga ili kuinua uzalishaji wa mazao na kipato | Wanakikundi wanaweza kufanya kazi kwa kujitolea Kulima mashamba na kupanda kwa kutumia mbegu zilizozalishwa na wanakikundi wenyewe | • Ukosefu wa mabomba ya umwagiliaji<br>• Ahadi za wafadhili kuwa wataleta mkopo na hawakuleta zimekatisha tamaa |
| Juhudi (1993) | Ibumila | Njombe | • Kuondoa tatizo la utapiamlo kwa watoto chini ya umri wa miaka 5<br>• Kuinua pato la kaya hasa akina mama<br>• Kujenga nyumba bora na kusomesha watoto | • Kikundi kina katiba<br>• Kikundi kina uongozi imara<br>• Kikundi kina wanachama wanaofuata mwongozo wa kikundi<br>• Kikundi kina ofisi<br>• Kikundi kina akaunti<br>• Kila mwanakikundi ana eneo | • Elimu duni ya ubunifu wa miradi ya kiuchumi na jinsi ya kuiendesha<br>• Baadhi ya wanakikundi kutofuata ushauri wa viongozi na wataalamu<br>• Mikakati<br>• Kuwa na vikao mara kwa mara ili kuwashauri |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | • Kupunguza tatizo la uhaba wa malisho hasa wakati wa kiangazi<br>• Ubunifu wa miradi ya kiuchumi ili kupunguza umaskini | di ana eneo la malisho kuanzia ekari 1-5 | wanakikundi<br>• Kuhamasisha kujiunga na SACCOs ili kujiwekea akiba zao |
| Juhudi (2001) | Kitanda | Mbinga | • Kuongeza uzalishaji wa mahindi kutoka gunia 5-10 kwa eka ifikapo 2005<br>• Kuinua kipato kuanzia 50,000 kwa kaya hadi 100,000 kwa mwaka | Kikundi kina akaunti yenye sh 70,000 na kiasi kitaongezeka baada ya kuuza mahindi gunia 15 yanayotarajiwa kuvunwa | • Ukosefu wa vitendea kazi mfano mabomba, mbegu n.k.<br>• Ushiriki usioridhisha wa wanakikundi |
| Wanyamakazi (2001) | Matai | Sumbawanga | Kufanya utafiti wa wanyamakazi na zana zinazotumika na wanyamakazi | • Wanakikundi wapo na wanaendelea kuimarisha kikundi muda wa miaka miwili<br>• Kikundi kinatambulika na wananchi pamoja na viongozi<br>• Kikundi kimeonesha mafanikio ya shughuli zinzofanyika<br>• Kikundi kinapata ushauri mara kwa | • Kikundi hakina malengo yanayoelewek a<br>• Kikundi hakina akiba<br>• Kikundi hakina uongozi imara<br>• Kuna ushirikiano mdogo kati ya wanakikundi<br>• Kikundi hakina katiba<br>• Mshikamano mdogo<br>• Wanakikundi kutoelewa vizuri malengo ya kikundi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mara kutoka kwa wataalamu na watafiti na sasa utaalamu uliotokana na utafiti umeanza kutumika na mtu mmoja mmoja mashambani | |
| Utafiti wa kilimo cha mpunga (2003) | Kikusya | Kyela | Kuiongezea jamii kipato zaidi/uzalishaji kutoka gunia 10 – 25 kwa ekari ifikapo 2009 Kila mwanakikundi alime hekta 1 kwa kushirikiana na wanakikundi wenzake na kutumia ujuzi uliofundishwa na wataalamu | • Wanakikundi kushirikiana katika kazi za shamba<br>• Kila mwanakikundi amelima robo tatu ekari baada ya utafiti<br>• Kikundi kina viongozi wanaoongoza kikundi vizuri<br>• Kikundi kina daftari la kumbukumbu<br>• Kikundi kina katiba ambayo haijapitishwa na wahusika | • Uwezo mdogo kiutendaji sababu kilizamia kwenye utafiti zaidi. Kikundi ndiyo kinaanza<br>• Kikundi kiliundwa bila kujua lengo<br>• Mvua haitoshelezi shughuli za kilimo cha mpunga<br>• Ardhi haina rutuba<br>• Ukosefu wa pembejeo mfano: bei ya mbolea pia ni kubwa<br>• Ugumu wa kupata pumba. zinapatikana kwa umbali wa kilometa 7<br>• Kipato kidogo cha wanakikundi |
| Wanyama-kazi (2003) | Kisilo | Njombe | • Kupambana na umaskini kwa | • Wanakikundi wana mshikamano | Wanakikundi kutofuata muda uliopangwa wa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | kuongeza uzalishaji wa mazao ya viazi mviringo, mahindi, ngano, kutoka gunia 10 hadi 20 kwa hekta na matumizi ya zana za kisasa<br>• Kikundi kina akaunti benki<br>• Kikundi kimejiunga na SACCOS | • Wanakikundi kutumia maksai katika usafirishaji kama vile kusomba mbolea kwa kutumia mikokoteni<br>• Kufundisha vijiji vya jirani juu ya matumizi ya zana za kisasa kwa mfano kulima kwa maksai au punda | kazi |
| Wika (2002) | Kankwale | Sumbawanga Mjini | Kila mwanakikundi kufuga kuku wa kienyeji kati ya 50 na zaidi ili kuboresha afya ya jamii na kuongeza kipato | Wanakikundi wanafuga kuku kufuatia maelekezo kutoka kwa wataalamu | • Magonjwa ya kuku<br>• Ugumu wa upatikanaji wa madawa ya kutibu na kukinga<br>• Baadhi ya wanakikundi kutegemea pesa kutoka kwa wafadhili na inapokosekan a hukata tamaa |

## 8.3 Kiambatisho Na. 3: MIPANGO YA UTEKELEZAJI WA KAZI WATAKAPORUDI MAKWAO

### KIKUNDI – WIKA: Kata ya Senga- WILAYA – Sumbawanga

| TATIZO NA HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbukumbu usioridhisha | Kuona kwamba vitabu mbalimbali vya kumbukumbu vinatumika katika vikundi | • Kutoa elimu ya utunzaji wa kumbukumbu.<br>• Kununua kasha la kutunzia kumbukumbu.<br>• Kununua vitabu vya kumbukumbu za wageni, fedha, mahudhurio na risiti. | Julai 2004<br>Sept 2004<br>Sept 2004 | Vikundi<br>Wataalam husika<br>Maendeleo ya jamii |
| Watu hawajui umuhimu wa kujiunga na kikundi | Vikundi vimeundwa na ni endelevu | Kuhamasisha wanakikundi | Agosti | Kikundi |
| Kutokuwa na katiba | Kuhakikisha kwamba katiba inakuwepo na inatumika ipasavyo | Kukusanya wanakikundi ili kutunga katiba | Oktoba | Wanakikundi na jamii |

### VIKUNDI VYA KIKUSYA – WILAYA: Kyela

| TATIZO AU HALI HALISI | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Hakuna ratiba ya kazi, sheria wala kanuni za kazi katika vikundi | • Ratiba ya kazi inakuwepo<br>• Sheria ndogo ndogo zinakuwepo | Elimu kwa wanavikundi kwa kufanya mikutano na wanavikundi ya kutunga sheria ndogondogo | Julai 2004 | • Wataalam<br>• Maendeleo/jamii<br>• Wanavikundi |
| | Vikundi viwe endelevu | Kutoa elimu kwa wanakikundi kuwa na malengo endelevu badala ya kulenga utafiti tu. | Sept 2004 | • Wataalam<br>• Ushirika,<br>• M/jamii,<br>• Wanavikundi |
| Hakuna utaratibu wa | Utaratibu wa kutunza kumbukumbu | Kutoa elimu ya uwekaji | Okt 2004 | • Vikundi,<br>• Wataalam wa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| kutunza kumbukumbu | unaanzishwa | kumbukumbu | | maendeleo ya jamii<br>• Kilimo |
| Utunzaji wa kumbukumbu usio wa kuridhisha | Kuona kwamba vitabu vya kumbukumbu vinatumika katika vikundi | Kutoa elimu ya utunzaji wa kumbukumbu<br>Kununua kabati la kutunzia kumbukumbu. | Des 2004 | • Vikundi<br>• Maendeleo/Jamii |
| Kikundi hakina katiba | Kuona kikundi na katiba inatumika | Kufanya mikutano na wanakikundi wa kutengeneza katiba | Okt 2004 | Vikundi maendeleo ya jamii |
| Wanakikundi kutohudhuria vikao | Kuwahamasisha wanakikundi kuandika mahudhurio ya vikao | Kuwahamasisha wanakikundi wahudhurie vikao<br>Kuwaelimisha wanavikundi kuhusu faida za vikao | Okt 2004 | Vikundi Maendeleo/jamii |

## KIKUNDI: WANYAMAKAZI – Kijiji:Kisilo: Kata: Uwemba - Njombe

| TATIZO AU HALI YA SASA | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Hakuna katiba | Kuwepo na katiba halali na inatumika | Kuitisha mkutano wa wanakikundi ili kutunga katiba | Julai 2004 | Wanakikundi<br>Wataalam |
| Mahudhurio ya wanakikundi katika vikao ni hafifu | Kuona kwamba mahudhurio ya wanakikundi yanakuwa mazuri | Kila mwanakikundi aelimishwe wajibu wake katika kikao<br>Kuzingatia sheria na kanuni za kikundi kwa wanavikundi wote wakati wa vikao au mafunzo | Oktoba 2004 | • Wanakikundi viongozi wa vikundi<br>• Wataalam wa maendeleo ya jamii |

## KIKUNDI: WANYAMA KAZI. Kijiji: Matai, Kata: Matai, Rukwa

| TATIZO AU HALI YA SASA | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbukumbu haupo | Kuona kuwa vitabu vya kumbukumbu vipo na vinatumika | Kutoa elimu ya utunzaji wa kumbukumbu kwa wanakikundi 5<br>Kununua vitabu vya kumbukumbu vifuatavyo; kumbukumbu za fedha, wageni, mahudhurio, leja, na risiti. | Julai 2004<br><br>Oktoba 2004 | • Wanakikundi<br>• Viongozi wa kamati ya maendeleo ya jamii |
| Kikundi hakina katiba | Kuwepo na katiba inayotumika | Kuitisha mkutano wa wanakikundi wa kutunga katiba ya kikundi | Julai 2004 | • Wanakikundi<br>• Viongozi wa kamati ya maendeleo ya jamii |
| Kikundi hakina malengo | Kikundi kina malengo ya kueleweka | Kukaa na kikundi ili kuandaa malengo yaliyo endelevu | Julai 2004 | • Wanakikundi<br>• Viongozi wa kamati ya maendeleo ya jamii |

## KIKUNDI: NARETISHO: Kijiji: Matebete- Kata: Chimala, Mbarali

| TATIZO AU HALI YA SASA | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbu-kumbu usioridhisha | Kuona kuwa vitabu vya kumbukumbu vipo na vinatumika | • Kutoa elimu ya utunzaji wa kumbukumbu kwa wanakikundi.<br>• Kununua vitabu vya kumbukumbu vifuatavyo: Kitabu cha fedha, wageni, mahudhurio, leja, | Julai 2004<br><br>Oktoba 2004 | • Wanakikundi<br>• Viongozi wa kamati ya maendeleo ya jamii |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | na risiti. | | |
| Kikundi kufanya kazi bila kufuata katiba | Kuona kwamba katiba ipo na inatumika | Kufanya mkutano wa kusisitiza matumizi ya katiba | Juni 2004 | • Viongozi wa kikundi<br>• Wanakikundi |
| Viongozi wa kikundi hawashirikishi wanakikundi katika kutoa maamuzi | Kuona viongozi wanawashirikisha wanakikundi katika maamuzi yote | Kufanya mkutano wa pamoja ili kuchagua viongozi wanaojali wanakikundi wote | Julai 2004 | • Wanakikundi<br>• Wataalamu<br>• Viongozi wa serikali ya kijiji |

## KIKUNDI: JUHUDI: Kata: Utiri, Mbinga

| TATIZO AU HALI YA SASA | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbu-kumbu usioridhisha | Kuona kuwa vitabu vya kumbukumbu vipo na vinatumika | • Kutoa elimu ya utunzaji wa kumbukumbu kwa wanakikundi<br>• Kununua vitabu vya kumbukumbu vifuatavyo: Kitabu cha fedha, wageni, mahudhurio, leja, na risiti. | Julai 2004<br><br>Oktoba 2004 | • Wanakikundi<br>• Viongozi wa kamati ya maendeleo ya jamii |
| Katiba ya kikundi kutotumika na wanakikundi | Kuona katiba inatumika na wanakikundi wote | Kufanya mkutano wa kusisitiza matumizi ya katiba kwa wanakikundi wote | Juni 2004 | Wanakikundi<br>Viongozi wa kikundi |
| Kutokuwa na ratiba ya kazi | Kuona kuwa ratiba ya kazi ipo na inafuatwa | Kufanya mkutano na wanakikundi ili kuandaa ratiba ya kazi | Juni 2004 | Viongozi wa kikundi<br>Wanakikundi |

## KIKUNDI: JUHUDI: Kijiji: Ibumila, Njombe

| TATIZO AU HALI YA SASA | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbu-kumbu usioridhisha | Kuona kuwa vitabu vya kumbukumbu vipo na vinatumika | • Kutoa elimu ya utunzaji wa kumbukumbu kwa wanakikundi<br>• Kununua vitabu vya kumbukumbu vifuatavyo: Kitabu cha fedha, wageni, mahudhurio, leja, na risiti. | Julai 2004<br><br>Oktoba 2004 | • Wanakikundi<br>• Viongozi wa kamati ya maendeleo ya jamii |
| Kutokuwa na ratiba ya kazi | Kuona kuwa ratiba ya kazi ipo na inafuatwa | Kufanya mkutano wa wanakikundi wote wa kuandaa ratiba ya kazi | Julai–Agosti 2004 | • Wanakikundi<br>• Viongozi wa kamati ya maendeleo ya jamii ya jamii |
| Ukosefu wa uelewa wa wanakikundi kuhusu kujiunga na SACCOS | Kuona wanakikundi wanajiunga na kuweka akiba zao kutoka wanachama 35-60 | Kufanya mikutano ya uhamasishaji kwa wanakikundi wote | Julai–Desemba 2004 | |

## Chuo chaMafunzo cha Wakulima Ichenga: Njombe

| TATIZO AU HALI YA SASA | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbukumbu usioridhisha | Kuona kuwa vikundi vinatunza kumbukumbu mbalimbali katika shughuli zao za kila siku na kuhakikisha vitabu vipo na vinatumika | Kutoa elimu ya utunzaji wa kumbukumbu mbalimbali kwa wanakikundi | Julai 2004 | • Mtaalamu<br>• Wanakikundi<br>• Viongozi wa kamati ya maendeleo ya jamii |
| Vikundi vingi siyo imara | Watumishi/wataalamu wana uelewa wa uendeshaji wa vikundi | Kufanya mrejesho wa warsha ya uendelezaji wa vikundi kwa wakulima na | Juni 2004 | Mtaalamu wa FTC |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | wataalamu wa Taasisi | | |
| Vikundi vingi bado ni dhaifu | Vikundi vinakuwa imara na endelevu | • Kutoa mafunzo juu ya uendelezaji shughuli za vikundi<br>• Kuhamasisha uundaji wa vikundi<br>• Uimarishaji wa uongozi wa vikundi | Augusti 2004 | • Mtaalamu FTC<br>• Viongozi wa kamati ya maendeleo ya jamii |

## Kata: Matai: WILAYA: Sumbawanga

| TATIZO AU HALI YA SASA | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbu-kumbu usioridhisha | Kuona kuwa vitabu vya kumbu kumbu vinatumka | • Kutoa elimu ya utunzaji wa kumbukumbu kwa wanakikundi<br>• Kununua vitabu vya kumbukumbu, km. Kitabu cha fedha, wageni, mahudhurio, leja, na risiti.<br>• Kutengeneza sehemu ya kutunzia kumbukumbu | Julai 2004<br>Julai 2004<br>Septemba 2004 | • Wanakikundi<br>• Viongozi wa kamati ya maendeleo ya jamii |
| Vikundi kutokuwa na malengo ya kueleweka | Kuona kwamba vikundi vina malengo yanayoeleweka | • Kutoa elimu kwa vikundi juu ya kuwa na malengo endelevu<br>• Kuwezesha vikundi kutengeneza malengo ya vikundi | Julai 2004<br>Julai–Agosti 2004 | • Wanakikundi<br>• Wataalamu |
| Vikundi kutokuwa na katiba inayoeleweka na kutoitumia | Kuona kwamba vikundi vina katiba inayoeleweka na inatumika | • Kuelimisha vikundi juu ya umuhimu wa kuwa na katiba<br>• Kuwezesha vikundi kutengeneza katiba | Julai 2004<br>Julai-Agosti 2004 | • Wataalamu<br>• Wanakikundi |

## Ileje Rural Development Trust Fund

| TATIZO AU HALI YA SASA | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Vikundi vingi siyo imara | Watumishi na wataalamu wapate uelewa wa matatizo ya uundaji wa vikundi | Marejesho wa warsha ya uendelezaji wa vikundi kwa watumishi wataalamu wa taasisi | Juni 2004 | • P. Kindimba<br>• Wagani IRDTF |
| Kutokuwa na malengo halisi katika vikundi | Vikundi kuwa na malengo yaliyo wazi, yanayotekelezeka na kupimika | Kutoa mafunzo ya uendelezaji wa vikundi kwa vikundi visivyo katika mtandao wa MVIWAI Wilayani Ileje juu ya kutengeneza malengo halisi | Julai–Oktoba 2004 | • P. Kindimba<br>• Wagani Maendeleo ya jamii<br>• Wanavikundi |
| Kutokuwa na taarifa /kumbukumbu muhimu za maendeleo ya vikundi | Kuwepo na kumbukumbu za maendeleo ya shughuli mbalimbali za vikundi | Kuelimisha vikundi jinsi ya kuweka kumbukumbu za kazi, mapato, matumizi na ufuatiliaji wa tathmini ya shughuli za vikundi | Novemba 2004 | • P. Kindimba<br>• Wanavikundi |
| Mitandao mingi ya wakulima siyo imara | Mitandao imara kuanzia ngazi ya kijiji, kata, tarafa, na wilaya | Kutoa mafunzo juu ya uongozi bora, tofauti kati ya vikundi na mitandao, na umuhimu wa mitandao kwa wanavikundi wote waliopo wilayani Ileje | Oktoba 2004 – Juni 2005 | • P. Kindimba<br>• Wagani Maendeleo ya jamii<br>• Wanavikundi |

## AGRICULTURE AND RURAL DEVELOPMENT ASSOCIATION - RUKWA

| TATIZO AU HALI YA SASA | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbu-kumbu usioridhisha | Kuona kuwa vitabu vya kumbukumbu vipo na vinatumika | • Kutoa elimu ya utunzaji wa kumbukumbu kwa vikikundi 2<br>• Kununua vitabu vya kumbukumbu vifuatavyo; Kitabu cha fedha, wageni, mahudhurio, leja, na risiti. | Julai 2004<br><br>Oktoba 2004 | • Mtaalamu<br>• Wanakikundi<br>• Viongozi wa kamati<br>• Maendeleo ya jamii |
| Vikundi vingi siyo imara | Kuona vikundi imara na endelevu | • Kutoa mafunzo kwa vikundi 2 juu ya uimarishaji wa vikundi, uendelezaji na uongozi bora<br>• Kuimarisha vikundi | June 2004 na kuendelea<br><br>Julai 2004 na kuendelea | • Mtaalamu<br>• Wanakikundi<br>• Maendeleo ya jamii |
| Vikundi kutokuwa na katiba ianayoele-weka | Vikundi kuwa na katiba inayoeleweka na kuitumia | • Kutoa elimu kwa vikundi 2 juu ya utengenezaji wa katiba<br>• Kutengeneza katiba | Juni 2004<br><br>Julai 2004 | • Mtaalamu Wanavikundi<br>• Wataalamu wa ugani, Maendeleo ya jamii |

## KIKUNDI CHA MOTOMOTO

| TATIZO AU HALI YA SASA | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji wa kumbu-kumbu usioridhisha | Kuona kuwa vitabu vya kumbukumbu vipo na vinatumika | • Kutoa elimu ya utunzaji wa kumbukumbu kwa vikikundi 2<br>• Kununua vitabu vya kumbukumbu vifuatavyo: Kitabu cha fedha, wageni, | Julai 2004<br><br>Oktoba 2004 | • Mtaalamu<br>• Wanakikundi<br>• Viongozi wa kamati Maendeleo ya jamii, Ushirika, |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | mahudhurio, leja, na risiti. | | |
| Utegemezi uliokithiri hasa mikopo | Kuona wanavikundi wana miradi ya uchumi iliyo endelevu | • Kutoa mafunzo ya uongozi na kujitegemea<br>• Ubunifu na usimamizi wa wa vikundi miradi ya vikundi (watu 30) | Agosti 2004<br>Agosti 2004 na kuendelea | • Vikundi<br>• Wataalamu<br>• Viongozi wa vikundi |
| Uongozi wa vikundi siyo imara | Kuwa na uongozi imara | • Kuitisha mkutano wa wanakikundi wote ili kuchagua viongozi bora<br>• Kutoa elimu juu ya uongozi bora | Agosti 2004<br><br>Agosti 2004 na kuendelea | • Wanavikundi wote<br>• Wataalamu mbalimbali na viongozi wa vikundi |

# VIKUNDI KUTOKA WILAYA YA SONGEA VIJIJINI

| TATIZO AU HALI YA SASA | MABADILIKO YANAYOTARAJIWA | AINA YA KAZI ITAKAYOFANYIKA | KUANZIA | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| Utunzaji mbaya wa mali za kikundi | Kuona kwamba hakuna utumiaji mbaya wa mali ya kikundi | Kuweka vikao vya kikundi ili kupata taarifa ya mapato na matumizi ya kikundi | Julai 2004 | • Viongozi wa kikundi<br>• Wanakikundi |
| Kutokuwa na ratiba ya kazi kwenye kikundi | Kuhakikisha kuna ratiba ya kazi ya kikundi | Kufanya vikao vya kuandaa ratiba ya kazi | Julai 2004 | • Wanakikundi<br>• Viongozi wa kikundi |
| Utunzaji wa kumbukumbu usioridhisha | Kuona kwamba karatasi zote zinazotolewa taarifa zinatunzwa katika faili | • Kutoa elimu ya utunzaji wa kumbukumbu kwa vikundi 2<br>• Kununua vitabu vya kumbukumbu vifuatavyo:<br>- Kitabu cha mahudhurio na cha risiti.<br>- Kununua faili na meza yenye motto wa meza (drawer) ya kutunzia kumbukumbu | Septemba 2004<br>Septemba – Oktoba 2004<br>Septemba – Oktoba 2004 | • Vikundi<br>• Viongozi wa kamati<br>• Maendeleo ya jamii |